Jiwe la Kiroho la kujengea No. 123

# Yakupasa Ujifunze Jinsi ya Kumkubali Mungu

*Yohana Mt. 1:1-3, 12-13*

*"Hapo mwanzo kulikuweko Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu ,naye Neno alikuwa Mungu. Huyu mwanzo alikuwako kwa Mungu.Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo Yeye hakukufanyika chochote kilichofanyika……Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, Ndio wale waliaminio Jina lake; waliozaliwa si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu.*

Hebu tusikilize kile ambacho Nabii wa Mungu amesema:
Ni Roho Mtakatifu leo anayetafuta mioyo iliyo miaminifu ambayo itaamini ujumbe. Kila kitu kilichoahidiwa katika Biblia ni kwa ajili ya muamini huyo na unapokubali kwa ukaminifu wake. Naye Mungu anajua utafanya hilo; Naye anakupa wewe hati ya (uthibitisho kwa kumpokea Roho Mtakatifu), kama aliye tengwa kwa hilo. Na sasa kila ahadi iliyo ahidiwa iko kwenye uwezo wako wa kuipata na Roho Mtakatifu yuko pale kuihuisha kwako.Ooh mimi. Tunapaswa kuwa watu wa namna gani? Jinsi ilivyo ya ajabu kuona Roho Mtakatifu wa Mungu aliye mkuu yupo hapa kudhihirisha uwezo huo. Fikiria hilo.

Kijana mdogo ambaye hajawahi kutembea, atajaribu kutembea chini hapa kwenye upande wa marefu wa kanisa hapa, ataanguka mara kumi na mbili na kuchoka kabla ya kufika hapa.Bali yoyote ajuaye kutembea,mwana riadha, atatembea upande huo wa marefu ya kanisa bila kuona kitu, anacho hicho kwa kuanzia, naye ndivyo alivyo sasa.

Hivyo ndivyo alivyo hasa na kuhubiri uponyaji wa kiungu au chochote kile. Kwa kadiri unavyo endelea, unaanza kujifunza. Kama hujifunzi, kuna kitu hakiko sahihi, unaona? Yakupasa ujifunze, na yakupasa ujifunze jinsi ya kumkubali Mungu na vile ambavyo hasa inamaanisha.
Sasa "Imani'' ni "Ufunuo utokao kwa Mungu''. Sasa "Imani'' ni "Ufunuo.Hapa ndipo nipendapo nikae kwa kitambo. Ni ufunuo. Amekufunulia wewe kwa neema yake. Siyo chochote ulichokifanya. Hukuwa na kazi yoyote yako ili kukuletea imani. Hukuwa na imani umepewa hiyo kwa neema ya Mungu(1 Petro 1:13 ). Na Mungu ataikufunulia; kwa hiyo imani ni Ufunuo (Mathayo 16:17-18) na kanisa lote la Mungu linajengwa juu ya Ufunuo.

Kuzungumza Neno ni mtu; kuthibitisha Neno ni Mungu. Kusema jambo fulani, ni kitu kimoja; Mungu kulitenda hilo, ni jambo lingine Mungu hahitaji mtafsiri,Yeye hufanya tafsiri yake mwenyewe.

Sasa tunajiandaa kuwa na mstari wa maombi kuombea wagonjwa,Mungu akipenda.Na tunajua kwamba hakuna hata mmoja,mwanaume, mwanamke, mwanadamu au Malaika yoyote awezaye kuponya, kwa maana Mungu tayari amefanya hivyo. Amefanya maandalizi, jambo moja tu uwezalo kufanya ni kulipokea hilo.

Hakuna mtu, Malaika wala chochote, hata Mungu mwenyewe awezaye kukusamehe dhambi zako.Imekwisha kutendeka .Yesu alifanya hilo pale Msalabani (Waefeso 1:7).Lakini kamwe haitakusaidia au kukupa faida yoyote, mpaka umeikubali.

Sasa kama ningalikuwa Bwana Yesu nisimamaye hapa, na mwanamke huyu ni mgonjwa, unajua nisingeweza kumponya kama ningekuwa Bwana Yesu. Nisingeweza, kwa sababu tayari nimeshafanya hilo.Sasa wangapi wanajua hilo ni kweli hakika.Yeye ameshasamehe kila dhambi. Yeye ameshaponya kila mtu mgonjwa.Yeye tayari ametoa ile damu pale msalabani.Gharama tayari imelipwa.Yote imelipwa (1Petro 1:18-20).Lakini jambo moja likupasalo ni kuikubali.Kuiamini na kuikubali.Na huwezi kuikubali, mpaka kwanza umeiamini.Unaona? Amini injili.

Sasa hapo ndipo ambapo watu wanafikiria leo juu ya uponyaji wa kiungu au kazi yoyote ya Mungu, kwamba kuna kitu inakupasa ufanye. Wewe, hakuna chochote cha kufanya ila kuamini, kumuamini Mungu tu.

Na, hilo, bado tunaliona miongoni mwa wanadamu, tunakuwa kwenye wazo hilo "kwamba kuna kinacho tupasa kufanya''.Twajisikia hivyo, kwamba tunacho cha kufanya pia.Wewe unacho cha kufanya kwa hilo; ni kusalimisha kabisa matakwa yako mwenyewe, mawazo yako na uchukuwe mapenzi ya Mungu na mawazo yake, na hilo limekwisha. Hilo ndilo lililopo. Chukua tu ahadi yake, usifikirie chochote kile.Tembea nalo, na Mungu atafanya yaliyobakia.

Ndipo walipotaka sheria.Na Mungu siku zote anakupa haja ya moyo wako; ameahidi (Kutoka 19:1-8).Lakini tunaona ya kuwa walipogeuka hatua moja kutoka upande wa Mungu alioahidi mwanzo, huo ulikuwa ni mwiba katika nyama zao mpaka sheria ilipoondolewa, mpaka Yesu Kristo alipokuja naye akasulubiwa kuiondoa sheria (Wagalatia 3:13; 5:1-6)ilikuwa ni mwiba katika nyama.

Na chochote unachojaribu kufanya cha nafsi yako, siku zote kitakuletea aibu.Kitatenda kwa hasara yako. Muamini Mungu, na hilo latosha. Kile alichoahidi Mungu, "Mimi ni Bwana Mungu wako nikuponyaye na magonjwa yako yote"(Kutoka 15:26).Kama yuko mmoja wenu ni mgonjwa, na awaite wazee wa kanisa (Yakobo 5:14-16).Aliahidi kazi alizofanya zitafanywa ndani ya kanisa lake (Yohana 14:12).

Ninaamini kuwa Yesu Kristo amekukomboa kutoka kwenye maisha ya ugonjwa kama vile alivyokukomboa kutoka kwenye maisha ya dhambi. Kama lile agano la kale lilikuwa na uponyaji hata katika upatanisho ule wa zamani wa damu ya Kondoo, na mbuzi na ng'ombe ilikuwa na uponyaji, si zaidi sana agano hili lililo bora lina uponyaji ndani yake katika damu ya mwana wa Mungu, Yesu Kristo (Waebrani 8:6-10).

Sasa umekwisha kuponywa, kila mmoja wenu, lakini sababu ya pekee kwanini huwezi kuupokea, ni kwa sababu unataka kupitia kwenye utaratibu wa kuwekewa mikono.Hilo ni sawa.Lakini hilo halikupi uponyaji. Umeponywa kwa Imani yako katika kazi ya Mungu iliyomalizika pale Msalabani.(Isaya 53:4-5).Uponyaji wako unakuwa kupitia hilo.Sasa Roho Mtakatifu amekuongoza hapa usiku wa leo.Kwa nini? Uamini uponyaji. Kama kuna chemchemi iliyofunguliwa mahali,Anawajibika kukuongoza wewe huko.Kinachofuatia ni juu yako.

Ni jambo la kisiri unazaliwa ndani ya mwili wa siri wa Kristo.Hivyo ndivyo unavyoingia ndani Yake.

1Wakorinto, sura ya 12 (mstari 12-13). Mwili mmoja…tunaingiaje katika mwili huo? Kwa Roho mmoja tumebatizwa katika mwili mmoja. Na ukiwa ndani ya mwili huu, u huru, na uhakika wa ufufuo.Mungu amemtwika Yeye maovu yenu yote".(1Petro 2:24, Yohana 1:29). Sio kwa kupeana mikono, sio kwa barua moja ya kanisa, bali kwa Roho Mtakatifu mmoja,myahudi, mmataifa wa njano, mweusi, mweupe, wote tulibatizwa kwa Roho mmoja ndani ya mwili mmoja, kwa damu yake ya agano "Na nionapo damu,nitapita juu yako"(Kutoka 12:13) na tunawekwa huru na mauti, huru na maumivu, huru na dhambi. "Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, Kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake"(1Yohana3:9).Hapana dhambi……"Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yetu wa mbinguni alivyo mkamilifu" (Matayo 5:48). Yesu alisema mwawezaje kuwa wakamilifu? Huwezi kufanya hilo.Ulizaliwa katika dhambi, ukaumbwa katika maovu, ukaja ulimwenguni ukisema uongo.Lakini Unapomkubali Kristo kama ngome yako ya dhambi, unapomkubali Yeye kwa imani, ukiamini kwamba alikuokoa, na amekufa akachukuwa mahali pako, na kuchukuwa dhambi zako, ndipo Mungu anakukubali wewe na kukubatiza katika mwili na haoni dhambi zako tena. Nawezaje kuwa mwenye dhambi wakati ipo damu madhabahuni kwa upatanishi wangu?

Na pale Mungu aliponikubali na kunibatiza na Roho Mtakatifu anayo Imani na mimi ya kuwa sitatenda dhambi kwa makusudi. Kwa hivyo Mwanae alifanya upatanisho kwa ajili yangu, na siwezi kuwa mwenye dhambi ili mradi nimehesabiwa haki na amenichukuwa katika mwili wake; nimekombolewa Naye.Siyo kile nifanyacho bali kile alichofanya kwa ajili yangu. Hiyo ni Injili. Waefeso 4:30, amesema "wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa Yeye mlitiwa Muhuri hata siku ya ukombozi

Mhubiri mashuhuri wa kibaptisti aliniambia sio muda mrefu uliopita, alisema Ndugu Branham, Ibrahimu aliamini Mungu, na akahesabiwa haki. Angefanya jambo gani zaidi ila kumwamini Mungu? "tunaamini tunapokea Roho Mtakatifu tunapoamini".Nikasema lakini umekosea; pamoja na uaminifu wako umekosea.Paulo alisema katika Matendo 19, kwa wale wabaptisti waliokuwa na mchungaji mzuri juu pale, mwanasheria aliyeongoka, je mlipokea Roho Mtakatifu tangu mlipo amini? Akasema; kile cha mwanzo hakisemi hivyo" nikasema hivyo.Ninayo"Emphatic Diaglott" na nikasema hivyo hivyo katika kila tafsiri Kigiriki na kiebrania. Akasema, je ulipokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini (Efeso 1:13-14) nikasema "Ibrahim aliamini; hiyo ni kweli. Lakini Mungu alimpa ishara ya kuwa ameikubali imani yake, na akampa yeye mhuri ya kutahiriwa".hiyo ni kweli Yeye amemkubali kwa sababu amempa ishara ya kuwa amemkubali (Rumi 4:1-12).

Kama unasema unaamini na bado hujampokea Roho Mtakatifu.Mungu hajakutia muhuri bado,bado Mungu hajakuamini vya kutosha. Unapomjia Mungu,Mungu anakutia muhuri na Roho Mtakatifu mpaka siku ya ukombozi (Efeso 4:30) Na huo ni ujumbe wa kanisa Amina.

Kuna jambo moja nataka kuwa mwaminifu juu yake enyi marafiki. Njia ni ile ile Mungu anaponya kwa msingi kuwa utamtumikia Yeye unaona? Ni kwa msingi huo huo wa kumtumikia. Tunapokea uponyaji wetu kwa msingi huo huo tutamtumikia Yeye baada ya kuponywa.

Sasa, Biblia ilisema "ungamianeni dhambi zenu ninyi kwa ninyi (Yakobo 5:16) mpate kuponywa" unaona? Ni kwa msingi kuwa utamtumikia Mungu.Wengi wenu pengine wako kwenye hali ya kufa. Na ni lazima utakufa kama jambo fulani halikutendeka. Hivyo nakutaka ndani ya moyo wako…………..

Sasa tunaweza kukupaka mafuta;tunaweza kukuombea mchungaji wenu pamoja nami tuombe maombi ya imani, tufanye chochote tuwezacho.Lakini haitakusaidia mpaka wewe mwenyewe uingie kwenye ushirikiano na Kristo. Unaona? Lazima uje kwenye ushirikiano wa, "mimi,Bwana"

Huokolewi usiku wa leo; ulikuwa umeokolewa, ulikuwa umeokolewa miaka elfu moja na mia tisa iliyopita. Na sasa pengine usiku wa leo utaukubali huo wokovu, lakini ulikuwa umelipiwa tayari.Deni lililipwa.Na shetani alikuweka duka la rehani,Yesu akaja na kukukomboa na kufungua milango, na jambo moja tu la kufanya ni kutembea na kukiri uhuru wako.Hilo tu. Unayo tiketi kutoka kwa Mungu kwamba deni imelipwa. Yesu alisema katika maneno yake ya mwisho "imekwisha"(Yohana Mt. 19:30).Kila baraka ya ukombozi ilikuwa imekwisha kabisa.Hasira kuu ya Mungu juu ya dhambi,alipofanyika dhambi kwa ajili yetu 2Kor 5:21; (Isaya 61:1-3) ile deni ililipwa (Kolosai2:13-15).

Shetani hana nguvu zozote, anaweza tu kutishia kwa hizo.Kama anaweza kukutishia ukubali,hilo ni sawa inapasa uyapate.Lakini kisheria hana nguvu hata kidogo. Kila nguvu alizokuwa nazo alinyang'anywa pale msalabani.Pale ndipo deni ilipolipwa.Yeye sio chochote ila mtishiaji.Kama unataka kusikiliza vitisho vyake,vyema, hilo ni sawa.Lakini hulazimiki kufanya hivyo; uko huru usiku huu wa leo.Amekuweka huru.

Na sasa kama kitu fulani katika neno kitakufanya utambue kwamba uko huru kwa neema yake, au kama kitu fulani, kitambue, na Neno linakufanya uelewe, au tendo fulani la Mungu, kwamba hilo la kuhusu wewe,latuhusu sisi wote. Hapo unalikubali katika misingi hiyo,na unakuwa huru nawe.Sio lazima ujisikie tofauti;huhitaji kujisikia chochote hata kidogo.Msingi wake siyo…..Yesu hajasema je ulijisikiaje? Yeye alisema, "Je umeliamini hilo"? Hiyo ni imani. Hiyo ni imani yetu, ni mkono wenye nguvu ule ambao unashikilia Upanga wa Mungu ukatao kuwili (Waebrania 4:12-13) na huo upanga ukatao kuwili utakata kila ahadi bure, kama huo mkono wa imani una uwezo wa kuushikilia huo upanga.Watu wengine wana misuli dhaifu yenye matatizo pengine wanaweza tu kukata kamkwaruza kadogo, kanakotosha kujiunga na kanisa.Wengine wanaweza kufikiria kuhesabiwa haki kwa imani.Wengine njia yote mpaka kwenye ubatizo wa Roho Mtakati.Mkono mkuu wenye nguvu, unashikilia hii Biblia, unaweza ukakata kila ahadi bure. Hiyo ni kweli.Hivyo iweni hodari katika Bwana (Efeso 6:10).

Sasa, naweza kuiangalia ngano, ikiwa imekaa mkononi mwangu. Naitambua ni ngano. Naweza kusema hiyo ni ngano.Naweza kuonyesha udongo, na udongo kama ungeweza kuangalia ungesema "ndiyo, hiyo ni ngano.Naamini ni ngano, naamini kila Neno juu yake".Lakini ngano hiyo haiwezi kuzaa ngano, mpaka ianguke kwenye udongo na ife.Hiyo ni kweli.

Hiyo ni mtu anaye angalia, kikanuni, na kusema "ndio naamini uponyaji, naamini ni kweli. Naamini ni Neno la Mungu.Naamini ni kwa ajili ya mwaminio.Naamini ninayo imani ya

kulipokea hilo”. Lakini mpaka utakapolipokea.Unapata ninacho maanisha? Sasa unapolipokea, unalifurahia (1Wathesalonike 1:2-7).Lile Neno liko pale;hiyo imemaliza mashaka yote yamekufa; takataka zote zimedongoka; na maisha mapya yanachipua, yakikua kuendea uponyaji wako.Hapo ndipo hasa unapopata uponyaji wako. Hapo ndipo uponyaji unapotokea. Imani huja kwa kusikia, kusikia Neno la Mungu (Rumi 10:17).

Natamani tungeweza kuyapata mengi pale, kama tunge…kama ungelipa kwa kiasi.Sio imani ya kiakili lakini itokayo moyoni.

Hapo hakuna hata mmoja, hakuna popote, awezaye kukutingisha uliache hilo. Pale kitu Fulani kinapoweka nanga.Hiyo imekwisha.Huwezi kulikataa hilo tena kama vile usivyoweza kukataa kwamba wewe ni binadamu.Unaaona? ni ile sehemu ambayo ni halisi.Lazima tuliamini hilo.

Sasa napenda kusema hili, kwamba mimi sio mponyaji wa kiMungu.Watu wananiita hivyo.Lakini sivyo.Hakuna mtu aliye mponyaji, kama mtu anakuja na kusema ni mponyaji,wewe mwangalie mtu huyo: kuna kitu fulani siyo sahihi.Na pia mimi siyo Mwokozi.Siwezi kuwa Mkombozi kwa kadri ile ile nisivyoweza kuwa mponyaji. Kwasababu,Yeye,Kristo alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa kwake sisi tumeponywa.Ni jambo lililokwishapita (Isaya 53:4-5).

Kila dhambi duniani ilisamehewa Kristo alipokufa msalabani.Unaamini hili? Kuna damu ya upatanisho madhabahuni kwa ajili ya dhambi ya dunia.. Lakini haitakufanyia jambo lolote zuri mpaka utakapoikubali na kukiri.Na huwezi ukaifanyia kazi mpaka kwanza useme, na uikubali kwa imani.

Hapo sasa Yeye ni Kuhani Mkuu alifanya upatanisho juu ya ukirifu wetu (Waebrania 4:14-16; 3:1-6), unaona Hawezi kusogea,Amefungiwa;Hakuna chochote awezacho kufanya, mpaka kwanza amelikubali na kulikiri; na uliamini kutoka moyoni mwako.Hilo ndilo liwezalo kumgusa Yeye, na hapo anaweza kutenda kazi juu ya hilo na kufanya upatanisho kwa ajili yako. Ndiyo hivyo.

Sasa kumbuka, kila baraka ya ukombozi imekwisha kununuliwa. Ile gharama imelipwa. Kuna njia moja tu pekee uwezayo kuipokea hiyo,nayo ni kuiamini na kuikubali.Yeye ni kuhani Mkuu wa maungamo yetu. Kile kiebrania kinasema,Yale maandishi ya kiebrania yanasema, “Yeye ni kuhani Mkuu wa maungamo yetu” kuungama na kukiri ni jambo moja hilo. Yeye ni kuhani Mkuu wa maungamo yetu.Kwa hiyo hawezi kufanya lolote juu yetu mpaka kwanza tukiri ya kuwa Amekwisha kulifanya hilo.Nasa tunapokiri hilo hapo sasa Yeye anakuwa ni kuhani Mkuu, mpatanishi anayetenda kazi kulifanya hilo liwe sahihi.Kwa hiyo tunaomba tukimtumaini Mungu usiku huu wa leo, katika ukarimu wake na huruma, kwamba atatupa neema yake iliyo kuu usiku huu wa leo.Na sasa kumbuka yapasa ulikubali hilo.

Mwenye dhambi anaweza akaja hapa madhabahuni akiwa kijana mvulana au msichana katika umri wa miaka kumi na minne, nao wata kuletea chakula chako hapa,nawe umlilie Bwana hata ufikishe miaka tisini,hutaokolewa.Lazima kwanza ukubali kile alicho kutendea unaona? Inabidi ulikubali hilo wewe mwenyewe.Unapolikubali Yeye anakuwa ni kuhani mkuu, mpatanishi kufanya maombezi juu ya maungamo yako juu ya kile unacho amini.Imani halisi

haijui kushindwa.Kimekwisha kutendeka. Hilo limekwisha.Mungu amesema hivyo na hiyo inamaliza hilo unaona? Mungu amesema hivyo.

Sasa hilo ni jambo lile lile wakati wowote. Unapoamini hasa,hilo linamgusa. Sasa mwanamke yule mdogo aliyegusa vazi lake, alisema, “kama tu nitagusa vazi lake,nitakuwa mzima” (Marko 5:25-34). Naye akafanya hivyo, alipofanya vile imani yake ilivyomtaka afanye. Kumgusa Yeye, yeye aliisikia. Unaona? Naye akageuka, akazungumza naye. Sasa,Yeye ni yule jana, leo na hata milele.Kama tu utamwamini Kristo.Mwamini Yeye.Ukaache imani yako iguse vazi lake.

Na Yeye, sasa hivi ni Kuhani Mkuu anaye weza kuguswa na manyonge yetu.Tunajua hilo.Na kama ni Yeye yule jana, leo, na hata milele, anapaswa atende leo kama alivyotenda jana, kama Yeye ni kuhani mkuu sasa je hutaamini? Kuwa na imani na Mungu.

Tunasoma katika Waebrania 10:19-22 “Tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, njia ile iliyo mpya, iliyo hai……”Sio njia ya zamani, “kwa njia mpya iliyo hai….” Ilikuwa ni njia iliyo kufa, agizo la sheria; lakini sasa tunaingia kwa neema, kwa Roho Mtakatifu,Oh, Natumaini unaliona hilo.Sio chochote uwezacho kufanya sheria ilikuwa ni kazi, “Usishike, usiguse, usile nyama, shika Sabato, mwezi mpya,yote hayo ni aina za Ibada vile mtu amefanya lakini katika hii njia mpya na iliyo hai,” siyo chochote tuwezacho kufanya, ni kile alichotutendea sisi kwa neema. Tunakipokea,Kristo anaziondoa dhambi.Tunaamini hilo, tunasikia injili, tunaiamini,tunaikubali,na hivyo kama tumeikubali kweli, kutoka vilindi vya mioyo yetu.Mungu anatupa Roho Mtakatifu kama shahidi (Efeso 1:13-14).

Ndipo Roho Mtakatifu anakushuhudia kuwa dhambi zako zimeondolewa, na umekufa kwa mambo ya ulimwengu.Unafufuka katika upya wa maisha, kutembea maisha mapya, kuishi maisha mapya, kuishi katika nguvu na uwepo wa Mungu. Siyo kuchukuliwa na kila upepo tena;Lakini kutembea katika Roho kama wana na binti za Mungu (Rumi 8:1) imesema “sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu ambao wanatembea sio katika mwili bali katika Roho”.

Kuna tofauti kubwa kati ya kuliangalia Neno la Mungu na kulipokea Neno la Mungu. Wale wanaolipokea Neno, sio wale wanaolichunguza, lakini wale wanaolipokea Mungu aliwaongeza kanisani, wale waliookolewa. Walipata watu elfu tatu waliolipokea Neno (Matendo 2:37-41).

Sasa unaweza kulisikia Neno likihubiriwa.Unaweza kuliangalia na kusema hiyo ni kweli. Kaini alifanya hivyo wengine wote walifanya.Lakini pale Neno lilipoangukia hapo lilizaa.Wale waliolipokea, walibatizwa kwa furaha unaona? Kulipokea Neno..,..(Marko 4:20; Mathayo 13 :23,Luka 8:15;Yohana 17:6-8;Matendo 2:41;Yohana 1:12-13; 1Wathesalonike 1:4-6).

Sasa unapokea uvuvio ya kwamba Yesu Kristo alikufa kwa magonjwa yako,ni saa hiyo hiyo ambapo uponyaji wako unakujia.Hiyo ni kweli.Unapopokea kutoka mbinguni,kwamba Yesu alikufa kwa dhambi zako nawe umelipokea hilo,huhitaji tena maombi kwa ajili yako umeshalikubali na limemaliza hilo

Sasa tunaweza kuhubiri Neno,tukalielezea Neno.Lakini yakupasa ulipokee Neno.Oh haleluya. Hilo ndilo linaloliwasha moto ndugu.Unapolipokea, ule Ufunuo,kitu fulani kinakuja

toka kwa vile visivyoonekana, dunia ile ng'ambo. Kinakuja kikivingirika chini kupitia njia isiyoonekana mahali fulani ndani ya nafsi yako. Kile kinasema "sasa ninaliona hilo" macho yako yanawaka; midomo yako iliyo chini, inanyooka juu na kicheko.Kila nyama katika mwili wako yaonekana ikifurahi.Jambo fulani litaenda kutokea.Kitu fulani…..Huhitaji kuwa katika mstari wa maombi tena.Umekipata hicho sasa.

Hapa sasa tunapata kitu chote.Siyo msisimko, ingawa inaendana na msisimko.Ni kama tu vile nilivyosema: kuvuta na kulewa siyo dhambi;ni matunda ya dhambi. Inaonyesha huamini Unaona? Lakini kama kweli unaamini kutoka moyoni, na unajua kwamba….. katika msingi wa pale ulipokaa unalipokea kwa moyo wako wote,jambo fulani litaenda kutokea hapo hapo litatokea.nawe unaweza kusimama kama shahidi wa hilo, kwamba jambo fulani limetokea (Warumi 10:8-10).

Neno lote Mungu alilozungumza, lazima litimie, Mungu hawezi kusema chochote bila kukitimiza. Alipokwisha kulinena, nikazi iliyokwisha. Mungu akilinena ni lililokwisha kumalizika. Mungu kamwe hazungumzi mpaka awe tayari kwa hilo kutendeka na anapozungumza, ni kama kwamba limekwisha kutimia tayari. (Isaya 55:10-11,Isaya 46:9-11).

Sasa kama hilo halitupi msingi wa kuweka imani yetu juu yake. Mungu anaponena Neno, hilo tayari limekwisha. Je ni vipi juu ya ahadi zake ambazo ametuahidi? Kila kitu alichosema, tayari ni kazi iliyokwisha. Kwa hiyo tunapolipokea Neno lake mioyoni mwetu, linakuwa limetendeka, nalo limekwisha

Nukuu za Kiingereza

"Muhuri ya pasaka" uk. 19
"Imani ni kazi zilizodhihirishwa" Aya 98-105
"Nini kinachovutia kule mlimani?"Aya 156-158
"Kitendawili" (65-0117),Aya 72-77
"Kuongozwa na Roho"(59-0407) Aya 88-90
"vitambulisho vitano vya kanisa la kweli"(60-0911E), Aya 132-141
"Njia ya nabii wa kweli Aya E-110
"Nyuma ya pazia la wakati Aya 88-89
"Mara moja tena Bwana"(63-0120E) Aya 14-16
"Njia aliyoiweka Mungu ya kuponywa (54-0719A) Aya E-31, E-28-29
"Tunataka kumwona Yesu (62-0712) Aya E-17
"Kumwita Yesu kwenye kituko (64-0329e)Aya E-4,E-52-53
"Dhambi isiyo samehewa Aya 34
"Mabirika yavujayo (64-0726E) Aya 66
"Muhuri ya sita kitabu cha mihuri ukurasa 443
" Imetupasa kutimiza haki yote (61- 1001 m)Aya 83-84

---

*jiwe la kiroho la kujengea na 123 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*
*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa: Charles E. Y. Kanju,*
*Box 5138, Tanga*

*E-mail: chaelika@live.com*

*Cell.phone 0718 230098*

*0684 230098*